# HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO

Edited with the trial version of Foxit Advanced PDF Editor
To remove this notice, visit: www.foxitsoftware.com/shopping
Hakiuzwi!

## 7.2 MAJI

Vyanzo vya Maji vilivyopo katika Wilaya ni Visima Virefu 64 na Vifupi 6, Chemichemi 6, Mabwawa 3, Malambo 59, Matangi ya kuvunia maji ya mvua 80. Hali ya usambazaji maji safi na salama umefikia asilimia 36 ambapo inatarajiwa kufikia asilimia 48 ifikapo mwaka 2016.

Baadhi ya Miradi mikubwa ya maji inayotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto katika mwaka 2013/2014, 2014/2015 ni Mradi wa Maji wa Dosidosi, Loolera, Kona, Eseki pamoja na mradi mkubwa wa maji Chapakazi wa Vijiji 10.



*Mradi wa maji Kata ya Loolera*

## 7.3 AFYA

Halmashauri ina jumla ya Vituo vya Afya 23 vya kutolea huduma za Afya, kati ya hivyo Zahanati 17, Vituo vya Afya viwili na Hospitali ya Wilaya moja. hadi 201



*Kituo cha Afya Kata ya Ndedo*

## 7.4 MIUNDOMBINU

### 7.4.1 BARABARA

Halmashauri ina jumla ya kilometa 837.9 ambazo zinahudumiwa na Halmashauri yenyewe. Kilometa 525.4 ni barabara za Wilaya, kilometa 382.7 ni barabara za Vijiji, Kilometa 23.4 ni barabara zilizopo Kibaya Mjini. Katika mtandao huo wa barabara kilometa 34 ni za changarawe. Wilaya pia ina barabara zinazohudumiwa na TANROADS zenye urefu wa kilometa 263 na zinapitika wakati wote wa mwaka. Kuna mradi wa ujenzi wa barabara ya lami katika Mji Mdogo wa Kibaya ambao ni kilometa 3 kuanzia Makao makuu ya Wilaya kupitia katikati ya Mji wa Kibaya.



*Ujenzi wa barabara ya Lami katikati ya Mji wa Kibaya*

### 7.4.2 VIWANJA VYA NDEGE

Wilaya ina jumla ya Viwanja vya Ndege vitano ambavyo ni vidogo navyo ni Loolera, Partimbo, Irkiushibour, Makame na Engang'oengare.



*Ndege iliyobeba Watalii wanaofika kutembelea baadhi ya hifadhi za wanyama.*

# FURSA ZA UWEKEZAJI ZILIZOPO KITETO

## 1. VIWANDA VYA USINDIKAJI WA MAZAO YA MIFUGO.

Kutokana na fursa ya upatikanaji wa Mifugo uwekezaji wa Viwanda vya kusindika mazao yatokanayo na mifugo unafaa.



*Mifugo (mbuzi, ng'ombe na kondoo) ikiwa inasubiria maji Kata ya Kijungu.*

## 2. VIWANDA VYA USINDIKAJI WA MAZAO YA KILIMO.

Kutokana na fursa ya upatikanaji wa Mazao ya Kilimo uwekezaji wa Kiwanda cha kusindika mazao yatokanayo na kilimo kama vile unga wa sembe, mafuta ya alizeti, vyakula vya mifugo, utengenezaji wa biskuti na chokleti fursa hii ipo wazi kwa yeyote anayetaka kuwekezwa.



*Baadhi ya mashamba (mbaazi, mahindi na alizeti) katika Kata ya Kiperesa*

## 3. UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MADINI

Kutokana na upatikanaji wa madini kama vile Rubi, Redganet, Greentormaline, Rhodelight, White quartz. Fursa hii iko wazi kwa wawekezaji kuja kuchimba madini haya.




*Madini yaliyopo ni Ruby, Gametes, Scopolite, Rhodlight, Greeuchrome*

## 4. UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MISITU


Kutokana na kuwepo kwa upatikanaji wa miti kama vile Mpingo, Mninga, Mtondoro, Mkindu, Mlama, Mgunga, Mpilipili na mingineyo mingi ambapo Mbao, Magogo, Mkaa, Miti ya uchongaji vinyago hupatikana hapa fursa hii ipo wazi kwa wawekezaji.

Kutokana na kuwepo kwa msitu wa SULEDO wenye maua ya aina mbalimbali imekuwa ni kivutio kwa nyuki ambao hutengeneza asali, fursa hii inaweza kuwekezwa kwa ajili ya ufugaji wa nyuki na usindikaji wa asali.



*Mizinga ya Nyuki katika msitu wa SULEDO*

## 5. UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA UTALII



*Utalii wa uwindaji na upigaji picha katika hifadhi ya INDEMA*






**KIMETOLEWA MWAKA 2015 KWA MAWASILIANO**

Sanduku la Posta 98
Simu Na: 027-2552000
Nukushi Na. 027-2552020
Barua pepe: ded@kitetodc.go.tz
Tovuti: www.kitetodc.go.tz



*Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mh. Joel Bendela akiwa na viongizi wa Wilaya ya Kiteto katika ziara ya ukaguzi wa Maabara za Shule za Sekondari.*

*Kulia ni, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya* ***Bw. Bosco O. Ndunguru,***

*Watatu ni Katibu Tawala (W) Kiteto* ***Bw. Nicomus B. John,***

*Wanne ni Mwenyekiti wa Halmashauri Wilaya ya Kiteto* ***Mh. Lembile Lemalali***

## 1. UTANGULIZI

Halmashauri ya wilaya ya Kiteto ni kati ya wilaya sita zinazounda mkoa wa Manyara.Ilizinduliwa mnamo julai mosi 1974 ikiwa katika mkoa wa Arusha na baadae kugawanywa mwaka 1993 na kuwa wilaya mbili yaani kiteto na simanjaro ambapo mkoa wa manyara ulianza rasmi julai 2002 baada ya kugawanywa kutoka mkoa wa Arusha.

## 1.1 IDADI YA WATU NA UKUBWA WA WILAYA

Wilaya hii ina ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 16,685 ambazo zimegawanyika katika matumizi mbalimbali yaani Malisho na Uwindaji wa Kitalii kilometa za Mraba 11,111, Kilimo kilometa za Mraba 3800, Misitu kilometa za Mraba 1674 na eneo lililobaki lenye kilometa za Mraba 100 ni kwa matumizi mengineyo.

## 2.0 MIPAKA YA WILAYA

Wilaya ya Kiteto ipo kati ya Longitudo 360 15' hadi 370 25' Mashariki na Latitudo 40 31' hadi 60 03' Kusini, ambapo kwa upande wa magharibi Wilaya ya Kiteto inapakana na Wilaya ya Kondoa Mkoa wa Dodoma wakati Kaskazini inapatikana na Wilaya ya Simanjiro na kwa upande wa Mashariki inapakana na Wilaya ya Kilindi iliyopo Mkoa wa Tanga. Kusini Mashariki inapakana naWilaya ya Gairo ambayo ipo Mkoa wa Morogoro.

## 3.0 HALI YA HEWA

Wilaya ya Kiteto ipo katika mwinuko wa kati ya meta 1000 hadi 1500 toka usawa wa bahari, kuna misimu miwili ya hali ya hewa kwa mwaka ambayo ni Masika na Kiangazi. Masika huwa kati ya mwezi Disemba hadi Mei na Kiangazi kati ya Juni hadi Novemba. Wilaya hupata Mvua za wastani wa kati ya mm 500 – 650 inayonyesha kwa wastani wa siku 54 na Jotoridi la wastani wa nyuzi 220 kwa mwaka.

## 4.0 SHUGHULI KUU ZA KIUCHUMI

Wananchi wa Wilaya ya Kiteto hujishugulisha zaidi na Ufugaji, Kilimo, Biashara ndogondogo pamoja na Viwanda vidogovidogo hizi ndizo shughuli kuu za kiuchumi za wakazi wa Kiteto.

## 4.1 MIFUGO


Ufugaji katika Wilaya ya Kiteto ni ule wa Mfumo asilia (Pastoralism) ambapo wanyama wafugwao wengi wao ni wa asili wakiwemo Ng'ombe 316,319, Mbuzi 229,290, Kondoo 82,397, Punda 13,859, Kuku 47,603 na Nguruwe 1,926 kwa ujumla kiasi cha nyama tani 144,171 hupatikana kwa mwaka na huchangia 52% ya mapato ya Halmashauri ya Wilaya na huajiri zaidi ya 60% ya wakazi wote wa Wilaya. Kupitia wataalamu wa Mifugo wa Wilaya jumla ya Ng'ombe 2400 zimehamilishwa kwa mwaka 2014 ambapo kuna vituo 3 vinavyotoa huduma hii. Pia Wataalamu wa Mifugo wanatoa ushauri wa kitaalam juu ya Ufugaji bora, matibabu na chanjo za mifugo. Kuna Majosho yapatayo 29, Mabwawa 3 na Malambo 51 ambayo hutoa huduma za mifugo katika kipindi chote cha mwaka.



*Ng'ombe wakinywa maji katika mbauti Kata ya Kijungu*

## 4.2 KILIMO

Kilimo ni shughuli kuu ya pili kiuchumi ambapo Hekta 380,000 zinafaa kwa kilimo, hekta zinazolimwa kwa sasa ni 188,101. Mazao yanayolimwa ni Mahindi, Alizeti, Maharage, Uwele, Mbaazi, Ulezi na Ufuta. Mahindi ndiyo zao kuu la Chakula na biashara ambapo kila mwaka huzaliswa tani 126,630. Mazao mengine yanayolimwa kwa kiasi ni Viazi vitamu, Ngwara, Mtama na Karanga.



*Zao la mahindi Kata ya Kiperesa*

## 4.3 MALI ASILI NA UTALII

### 4.3.1 HIFADHI ZA MISITU



*Msitu wa SULEDO*

Wananchi wa Wilaya ya Kiteto wanautamaduni wa kuhifadhi mazingira tangu miaka ya zamani. Hivyo kuna baadhi ya Hifadhi kama vile SULEDO, EMBORLEY MURTANGOS , WMA – MAKAME pamoja na hifadhi ya Taifa ya Njoge. Hifadhi ya Msitu wa SULEDO una ukubwa wa hekta 167,400. Hifadhi hii imejaliwa kuwa na miti ya aina mbalimbali kama vile Mpingo, Mninga, Mtondoro, Mkindu, Mlama, Mgunga, Mpilipili na mingineyo mingi ambapo Mbao, Magogo, Mkaa, Miti ya uchongaji vinyago hupatikana hapa.

Hifadhi ya Jamii ya Emborley Murtangos ina ukubwa wa Hekta 75,463. Hifadhi hii ina uoto wa asili ulioambatana na Mbuga zaidi ya 13 na milima na vilima zaidi ya 23 pamoja na mabwawa ya asili zaidi ya 56 ambapo wanyama kama Swala, Digidigi, Twiga hupatikana katika hifadhi hii. Hifadhi ya INDEMA - WMA MAKAME ina ukubwa wa hekta 379,362. Ambapo wanyama wengi kama Swala, Twiga, Tembo, Nyati, Nyumbu Chui, Simba na wengine wengi. Hifadhi hii ni ya jamii na ina vitalu vine vya uwindaji ambavyo ni Irkiushbour, Talamai, Maasai East na Maasai West - Naibourmurtu.





*Wanyamba mbalimbali katika hifadhi ya INDEMA*

Eneo hili ni kivutio kikubwa kwa watalii na limekuwa likiingizia hifadhi hii fedha nyingi za kigeni. Katika eneo hili hupatikana baadhi ya wanyama adimu kama vile Swala Twiga "Generuk", Kanga wenye kofia "Crested Guinea Fowl" na Choraa "Oryx" .







*Swala twiga, kanga wenye kofia na Choraa*

### 4.3.2 UFUGAJI WA NYUKI

Ufugaji nyuki wakubwa kwa ajili ya kuvuna Asali na Nta hufanywa katika eneo la hekta 60 tu kati ya hekta 227,400 zinazofaa kwa ufugaji nyuki. Mizinga 25,140 (220 kisasa na 24,920) inatumika kwa kuzalisha tani 360 kwa mwaka. Shughuli hii hufanywa katika hifadhi ya SULEDO.



*Mizinga ya Nyuki katika msitu wa SULEDO*

### 4.3.3 MADINI

Madini yanayopatikana ni"Rubi", "Red Garnets", "Scoptile", "Rhodelight", Greentomeline, Quartz and "Greenchrome". Kwa sasa shughuli za uchimbaji wa madini hufanywa katika Kata za Kijungu, Loolera na Songambele kupitia makampuni ya Athumani Kuge & patners, M/S Platinum Ltd na Talamai Group.



*Madini aina ya Ruby, Gametes, Scopolite, Rhodlight, Greeuchrome*

## 5. UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Kuna Makampuni yanayotoa huduma ya usafirishaji wa Mizigo aidha kuna Stendi kuu ya Mabasi iliyoko Kibaya Mjini ambayo ndiyo kitovu ya mikusanyiko ya abiria wanaokwena maeneo mbalimbali kama vile Mkoa wa Dar es salaam, Morogoro, Dodoma, Arusha, Babati - Manyara na Tanga.



*Baadhi ya mabasi ya Kampuni ya Kamwana Express na Struggle line katika Stendi kuu ya Mabasi Kibaya Mjini.*

## 6. HUDUMA ZA KIBENKI

Huduma za kibenki kwa wananchi hutolewa na Taasisi/Makampuni kama vile NMB, CRDB (Fahari Huduma – Awaboma Saccos), Benki ya Posta, Vodacom (M-Pesa), Airtel (Airtel Money) na Tigo (tiGO-Pesa).

## 7. VIWANDA NA USHIRIKA

Kuna viwanda vidogo vidogo 6, vikundi vya usindikaji wa mazao ya kilimo 4, usindikaji asali 1, Kiwanda cha maziwa 1, Vyama vya Ushirika wa Mazao (AMCOS) 15, Vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) 21, VICOBA 80 pamoja na Tasisi za kukopesha kama vile FINCA, FAIDIKA, BAYPORT na TUNAKOPESHA LTD. Vyama,Vikundi pamoja na Taasisi hizi zimekuwa zikitoa huduma ya mikopo kwa wananchi wa Kiteto.



*Kikundi cha uzalishaji mafuta ya alizeti Kibaya - Mjini*

Uwepo wa Mina-da katika Wilaya ya Kiteto imekuwa ikichochea kasi ya mzunguko wa biashara na kupelekea kukua kwa shughuli za kiuchumi hususani biashara ya uuzaji wa mifugo pamoja na mazao.

## 8.0 HUDUMA ZITOLEWAZO NA HALMASHAURI.

Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto imeendelea kutoa huduma mbalimbali za Kijamii kwa wananchi wake hususani katika sekta za Mifugo, Elimu, Afya, Maji, Kilimo na Miundombinu.

### 7.1 ELIMU NA MICHEZO

Wilaya ina Shule za Awali 79 zenye jumla ya Wanafunzi 4,685 ambapo wavulana ni 2543 na wasichana 2146. Zipo shule za Msingi zipatazo 88 ambazo shule za Serikali ni 86 na Shule za binafsi 2 zenye jumla ya Wanafunzi 38,688 wavulana wakiwa 20,301 na wasichana 18,337 mikondo 859 na darasa la I-VII, kati ya shule hizo saba ni za bweni.



*Kamati ya fedha na mipango ikikagua ujenzi wa nyumba ya Mwl. Katika Sekondari ya Magungu.*

Jumla ya watu wazima 102 wako katika program zinazotolewa za Mukeja, Memkwa na Kisomo Chenye Manufaa. Wilaya ina jumla ya Sekondari 17 ambazo shule za Serikali ni 16 na Shule ya binafsi 1 zenye jumla ya wanafunzi 4022 kati yao wavulana wakiwa 2084 na Wasichana 1938. Wilaya ina Maktaba 1 ambayo imekuwa ikitoa huduma ya kujisomea kwa wanafunzi wa shule na watu wengine kwa ajili ya kuongeza maarifa. Maktaba hii ni ya kisasa kwani ina Kompyuta na wataalam.



*Moja ya timu za mpira wa netiboli na mpira wa miguu Mjini Kibaya.*